Kueleza Imani Yako Kuhusu Ngono Kati ya Watu wa Jinsia Moja

Tumia daftari hili kufikiria njia bora za kueleza imani yako.

"Maneno yenu na yawe yenye neema sikuzote, . . . ili mjue jinsi mnavyopaswa kumjibu kila mtu."—Wakolosai 4:6.

1

KABLA YA KUJIBU, ZINGATIA HILI:

Wakati mwingine watu wanaposema Biblia imepitwa na wakati, wanachomaanisha *hasa* ni kwamba viwango vya Biblia vinatofautiana na viwango vyao. Unafikiri mtu unayezungumza naye anahisi kwamba viwango *vyote* vya Biblia vimepitwa na wakati—kutia ndani mambo inayokataza kama vile wizi, uzinzi na uuaji?—Waroma 13:8-10.

Ni mambo gani yanayofanya mtu huyo aamini hivyo?	Ni maswali gani utakayomuuliza ili kujua mambo mengine anayofikiria?	Unaweza kumsomea andiko au maandiko gani?

TAYARISHA JIBU LAKO

"Viwango vya Biblia vimepitwa na wakati!"

"Watu fulani husema hivyo. Lakini nina maoni tofauti na wao kwa sababu . . . "

_____

_____

_____

www.jw.org © 2016 Watch Tower Bible and Tract Society of Pennsylvania

2

“Wanaofanya ngono ya jinsia moja hawawezi kubadilika—wamezaliwa wakiwa na tamaa hiyo.”

KABLA YA KUJIBU, ZINGATIA HILI:

Biblia haisemi kama tamaa ya kufanya ngono ya jinsia moja ni ya kurithi au la. Hivyo badala ya kubishana kuhusu *chanzo* chake, kazia uangalifu *zoea* lenyewe.

Fikiria mifano ifuatayo. Ni mazoea gani mengine yanayoweza kukita mizizi? Kwa mfano, Methali 29:22 inasema kwamba baadhi ya watu ni *‘wenye* hasira’ na *“mwelekeo* wa ghadhabu.” Mtume Paulo hata alieleza hisia zake aliposema hivi: “Ninapotaka kufanya yaliyo sawa, yaliyo mabaya yapo pamoja nami.” (Waroma 7:21) Je, kila mara tunapaswa kutenda kulingana na tamaa tunazohisi?

Ni mambo gani yanayofanya mtu huyo aamini hivyo?	Ni maswali gani utakayomuuliza ili kujua mambo mengine anayofikiria?	Unaweza kumsomea andiko au maandiko gani?
_____	_____	_____
_____	_____	_____
_____	_____	_____

TAYARISHA JIBU LAKO

“Wanaofanya ngono ya jinsia moja hawawezi kubadilika—wamezaliwa wakiwa na tamaa hiyo.”

“Biblia haisemi kama tamaa ya kufanya ngono ya jinsia moja ni ya kurithi au la. Mambo *inayoeleza* ni . . . ”

_____

_____

_____

www.jw.org © 2016 Watch Tower Bible and Tract Society of Pennsylvania

3

KABLA YA KUJIBU, ZINGATIA HILI:

Je, inawezekana mtu huyo ana rafiki au ndugu ambaye ni shoga au msagaji? Je, mtu huyo anafikiri kwamba unapokataa *mazoea* ya mtu fulani inamaanisha unamkataa mtu *huyo?* Je, mtu huyo *anaelewa* kikamili maoni yako kuhusu ngono kati ya watu wa jinsia moja?

Pia: Je, wengine wanakuvumilia ikiwa wanatarajia ubadili maoni yako yafanane na yao?

Ni mambo gani yanayofanya mtu huyo aamini hivyo?

Ni maswali gani utakayomuuliza ili kujua mambo mengine anayofikiria?

Unaweza kumsomea andiko au maandiko gani?

TAYARISHA JIBU LAKO

“Unapaswa kubadili maoni yako kuhusu ngono kati ya watu wa jinsia moja.”

“Ninaweza kuelewa kwa nini unahisi hivyo. Hata hivyo, . . . ”

Kwa madokezo zaidi, ona *Maswali Ambayo Vijana Huuliza—Majibu Yafanyayo Kazi,* Buku la 1, Sura ya 23: “Ninaweza Kuelezaje Maoni ya Biblia Kuhusu Ugoni-Jinsia-Moja?” Kitabu hiki kinapatikana kwenye tovuti ya www.jw.org/sw. Angalia kwenye MACHAPISHO > VITABU na BROSHUA.

www.jw.org © 2016 Watch Tower Bible and Tract Society of Pennsylvania